MUHTASARI WA MKUTANO WA SULLIVAN
TAREHE 02 – 06/06/2008 ARUSHA

Mkutano huo ilihudhuriwa na wajumbe kutoka nchi mbalimbali za Afrika na Waafrika Diaspora na ulifunguliwa na Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete Raisi wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwajulisha wajumbe madhumuni makubwa ya Mkutano huo ni mawili:-

1. Katika kusheherekea siku ya 'The Rich Life of Great Pan Afrika Visionary Leader Latter Rev. Leon H. Sullivan' kuweka kumbukumbu hai ya Waafrika Diaspora na waafrika wa Bara la Afrika kwa ajili ya ushindi wa kweli katika kupigania haki za waafrika.

2. Kujenga daraja la ubia katika uwekezaji kati Waafrika Diaspora na marafiki wengine wa Afrika kwa ajili ya faida ya Afrika, ili kujenga mahusiano makubwa ambayo yataunganisha Afrika na Diaspora katika kuelezea changamoto zinazozikabili na mikakati ya kushughulikia changamoto hizo.

Majadiliano ya pamoja 2/6/2008: Afrika katika uchumi na Dunia (Afrika ni Global Economy):-

Majadiliano ya mada hiyo yaliongozwa na Balozi Andrew Young kuhusu jinsi Afrika itakanyoweza kuingia katika uchumi wa dunia kwa kuangalia utajiri wa Afrika kufuatana na raslimali nyingi zilizopo ambazo hazipo katika bara mengine dunia, lakini zipo changamoto ambazo zinasababisha Afrika kushindwa katika uchumi wa dunia, changamoto hizo zinatakiwa kuwekewa mikakati ya kubaliana nazo.

Balozi Andrew Young aliwambia wajumbe kwamba Nchi ya Tanzania na Bara la Afrika lina rasilimali nyingi za ardhi kwa ajili ya kilimo, madini, utalii, uvuvi, maliasili na kadhalika. Changamoto kubwa zinazazokabili Afrika ni pamoja na vita, maradhi ikiwemo ukimwi, umaskini, rushwa ufisadi na kadhalika vinafanya uchumi wa Afrika kushindwa kukua katika uchumi wa dunia.

Mikakati iliyopendekezwa na wajumbe ni pamoja na nchi za Afrika kuwa na sera maalum kuhusu jinsi ya kufanya uchumi wa nchi za Afrika kukua katika uchumi wa dunia kwa kutumia fursa zilizopo na kwa kuweka kado tofauti za siasa, utamaduni, vita, vile vile katika kupambana na kutokomeza maradhi, rushwa, ufisadi na viongozi kuondoa ubinafsi wao kwa kuungana pamoja katika kujenga uchumi imara kwa bara la Afrika.

Aidha waliwaomba Wamerikana wa asili ya Kiafrika na marafiki wengine wanaoipenda Afrika kusaidia na kuipa nguvu ili kujenga uchumi na kuboresha maisha ya waafrika hata hivyo Wamerikani Waafrika waliwataka Waafrika wote kuwafanya biashara kwa kufuata taratibu, miiko ya biashara duniani, kwa kufanya kazi ili kuendelea katika kujua na kutambua "goals" za muda mrefu

katika kukuza uchumi na kingia katika uchumi wa dunia, kutangaza fursa za afrika na kuzinadi kwa Daspora na marafiki wengine wa Afrik,vilevile kuchukua faida na manufaa ya mkutano wa nane wa Taasisi ya Sullivan katika kujenga Afrika kama njia ya kuweza kusaidia katika kukuza uchumi wetu, kuwa na ushirikiano/ubia wa kibiashara na Wamerikani asili ya Afrika na Marafiki wa Afrika kuwekeza katika rasilimali zilizopo na katika huduma za jamii kikamilifu.

MADA YA FURSA ZINAZOTOLEWA NA AGOA.Mada hii iliongozwa na Mr Gregory Simpkins wa Leon H. Sullivan Foundation

Mwendesha mada alianza kwa kuelezea wajumbe jinsi soko la AGOA linavyotoa upendeleo kwa bidhaa mbalimbali zilizoongezwa dhamani kutoka Afrika kwenda Merikani kwa kuuza bila kodi au ushuru wa aina yote.Wafanyabiashara wa Tanzania na Afrika wanatakiwa kutumia fursa nzuri za mpango AGOA katika kuuza bidhaa zao katika masoko ya Merikani kwani soko hilo nilipo kwa ajili yao katika kusaidia kukua kwa maendeleo ya uchumi wa Afrika, fursa hiyo inatakiwa kuichangamikiwa kwa kuuza bidhaa na katika kukuza uchumi wa Afrika.
Taarifa zilitolewa kuhusu mafanikio kubwa yaliyopatikana katika soko la AGOA kwa nchi za Boswana, Maritius na Madagascar kwa jinsi nchi hizo zilivyoweza kufanikiwa katika kuweka utaratibu mzuri katika kutumia fursa hizo kwa serikali kutekeleza masuala yafuatayo;

Kuthibiti “exchange rates”
Serikali ziliwasaidia wafanyabiashara mitaji na vifaa kwa ajili ya huduma za uchumi na jamii.
Vivutio vilitolewa kwa wawekezaji wa ndani na nje
Serikali iliwekeza katika elimu na miundombinu
Viwanda vya EPZ vilizalisha bidhaa zilizokubalika kwenye soko la AGOA
Bidhaa za EPZ zilitangazwa kwenye soko la AGOA.
Sera nzuri za serikali katika kuhakikisha EPZ inaendeshwa kwa faida.

Mada ya “Corporate Social Rensiponsibility, Global Sullivan, Principles and Development in Afrika” mada hii ilielezea umuhimu wa “corporate social responsibility” wajibu na uwazi wa serikali katika kusimamia biashara ili kuboresha maendeleo ya uchumi wa waafrika Mada ya Corporate Social Responsibility, Globas Sulluvan, Principles and Development in Afrika – mada uliyoongoza na Bernard anderson, Wharton School of Business Phindeiphing PA, USA.

Semina hii itajadili umuhimu wa kukua, “ Social respansibility, Business and Government accountability and transparency in commercial transcations to doing business in Afrika. Mada hii iliongozwa na……”. kwa watoa mada walielezea mambo muhimu ya kuzingatia katika kuanzisha kampuni katika mazingira au sehemu biashara na jamii iliyo karibu katika muhimu kwa biashara na Serikali,

wafanyakazi, wateja na Jamii kwa ajili ya manufaa ya kampuni katika kuzingatia sheria, sera, taratibu mbalimbali, aidha katika kutoa haki sawa kwa wafanyakazi wote, kwa sababu wao ndio wazalishaji vile vile kuwa na mahusiano mazuri na jamii biashara katika kutunza mazingira, kuchangia katika huduma za jamii za ujenzi wa miundo mbinuna huduma za afya, kuchangia katika elimu,katika kufanya hiyo unajenga mazingira mazuri ya kampuni kwani jamii hiyo ndiyo wanunuzi wa bidhaa /wateja wa bidhaa zitakazozalisha.

Meneja wanatakiwa kuzingatia matakwa ya wanahisa katika kutoa na kuchangia huduma za jamii bila kuathiri utendaji wa kiwanda/kampuni kwa kuhakikisha faida inapatikana kwa manufaa ya wenye/wanahisa na jamii kwa ujumla.

Kampuni itafanikiwa tu kwa sababu ya mahusiano mazuri na jamii iliyoizunguka na wafanyakazi kwa “interest with” za kufanya uzalishaji na shughuli za biashara, hazina kufanya katika kutia umuhumu wa mazingira ya biashara kama ni muhimu kwa mafanikio katika uzalishaji/biashara. Kukua kwa kampuni/biashara kutatengemea mafanikio katika ushirikiano na wadau wa karibu .

Serikali inatakiwa kuweka sera na sheria zenye vivutio na mazingira mazuri, wakuu wa Mikao wanapaswa kuyatilia mkazo ili kuvutia uwekezaji mikoani kwa makampuni mbalimbali yanayotaka kuwekeza katika fursa mbalimbali zilizopo mikoani.

MADA- Mjukumu ya Vijana katika kujenga uchumi wa Afrika kwa maisha ya baadaye. Mada hii iliongozwa na Frank Ski V-103 Atlanta/Frank Ski Kids Foundation.

Mtoa mada alianza kwa kusema kwamba wastani asilimia 21(%) ya Vijana hawana kazi kufuatana na Shirika la Kazi duniani wenye umri wa kati miaka 15 – 24. Vijana wana umuhimu na matumaini makubwa na ndiyo viongozi wa kesho.

Vijana wa Tanzania na Amerikani Waafrika kwa pamoja waliweza kufanya majadiliano na wawasilishe wa Afrika wa ujasiriamali wa vijana (youth enterpreneurs), katika kuwekeza katika michezo katika kuboresha uchumi wa Afrika na kazi nyingine ili kupata ubunifu katika mikakati ya kutatua vikwazo vinavyowakabili na kutafuta njia za kuwasaidia vijana katika uzalishaji mali kwa

kutumia fursa zilizopo katika ili kuingia katika uchumi wa dunia katika kutekeleza majukumu yafuatayo;

- Vijana wanatakiwa kuwa wenye maono na ubunifu katika kukuza uchumi wa Afrika
- Vijana wanakuwa kuwa wavumbuzi wa vitu mbalimbali vitakavyoweza kukuzwa uchumi wa afrika
- Vijana wanaweza kuleta mabadiliko mbalimbali ya uchumi katika Afrika kwani wao ndiyo viongozi wa baadaye
- Vijana wanakubalika na ni nguvu kazi katika kuendesha shughuli mbalimbali za uchumi.

Vijana wanaweza kuwa Viongozi wa kesho:

Kuwa vijana wajasiriamali – 'Young Enterprenuers skills'

- Vijana kuanzisha biashara mbalimbali
- Kuwa na mahusiano na vijana Diaspora na Marafiki wengine wa Afrika katika majadiliano mbalimbali na katika mahusiano ya michezo
- Vijana kushiriki katika kwa shughuli za uchumi na Jamii kwa ujumla
- Ushirikiano wa karibu kati ya vijana wa Afrika, diaspora na Marafiki waafrika katika kuwajengea vijana uwezo wa kuwawezesha kuwa viongozi wa baadaye.

Tarehe 03/06/2008:
Mkutano wa pamoja Afrika (Plenary) kuhusu kuboresha upatikanaji wa nishati ya umeme Afrika, ma hiyo iliongozwa na Ndugu Mark Digby wa General Electric Capetown, South Afrika.

- Afrika ni nchi yenye vyanzo vingi ya upatikanaji wa umeme lakini ndiyo nchi yenye upatikanaji wa umeme kidogo kwa umeme wa kisasa.majadiliano yalihusu mapendekezo na mipango ya namna ya kuongeza, kutawanya nakusambaza umeme kwa kutumia umeme mbadala, mpango huu ilijdiliwa kwa kuhusisha wawakilishi wa vyombo vya fedha vya kimataifa kwa ajili ya kufadhili umeme na miundo mbinukatika miradi ya Afrika katika Kuboresha upatikanaji wa nishati Afrika na jinsi ya kusaidia makampuni yanayotoa huduma za Umeme Afrika

  Mada-hii ilizungumzia changamoto, hali ya umeme Afrika na mikakati ya kukabiliana na changamoto za umeme katika bara la Afrika

Changamoto:

- Kukosa fedha za kuwekeza katika huduma za Umeme
- Technolejia ndogo katika kuboresha umeme wa gasi
- Kukosa vitendea kazi kwa ajili kupata wa gasi

- Kupanda kwa mafuta ya nishati

Hali ya Umeme Afrika:

- Asilimia 25 (%) tu wanatumia umeme kutokana na sababu mbalimbali kama zifuatazo;
-
- Kupanda kwa mafuta ya nishati
- Vita vya nchi na nchi na vya kikabila
- Kuongezeka kwa idadi ya watu
- Kuongezeka kwa uwekezaji katika viwanda na biashara
- Mipango mibovu na fedha kidogo kwa ajili ya umeme
- Hakuna ushindani katika huduma ya kutoa umeme (Kampuni)
- Gharama za umeme kuwa kubwa sana
- Sera za taratibu za Umeme hazipowazi na kuzielewa.
- Kushindwa kutoa huduma nzuri
- Uzalishaji kidogo wa Umeme
- Uchakafu wa mitambo
- Gharama kubwa katika Kutengeneza na kusambaza umeme

Mikakati:

- Kuboresha nishati, na Serikali kutumia mali zilipo kuongeza nishati ya Umeme
- Kuboresho kwa sekta binafsi katika kufanya kazi kwa ufanisi
- Kuongeza zaidi nishati kufuatana utaalaamu na kubadilisha mfumo wa umeme.
- Kuwa na mchanganyiko wa Umeme/Nishati mabadala, kama umeme wa jua, upepo, gasi, biagas, maji n.k.
- Kuwa na waafanyakazi/Meneja hodari na wa ubunifu katika kukabiliana na vikwazo vya umeme
- Kupunguza gharama Tariffs" katika nishati

Mada ya jinsi kuunganisha Nishati ya umeme wa njia mbili au zaidi mfumo wa Umeme (Power Pool) kati ya nchi na nchi.

Mada hii iliongozwa na Carolyn Haylock- kutoka Washington DC, US, kwa kwaeleza wajumbe wa mkutano kwa nchi ya kwanza katika Afrika kwa na umeme wa mfumo wa njia zaidi ya mbili ni South Afrika na baadaye nchi za Magharibi, East na Central na USAID imekuwa mstari wa mbele katika kufadhili kuchagua, kendeleza, kutoa na kupitisha kwa ajili ya matumizi ya baadaye ya nishati ya umeme kati ya nchi na nchi.

Viongozi wa nchi za kusini mwa Sahara katika warsha hiyo walizungumzia jinsi umeme wa 'four power pools' ulivyounganishwa kutoka nchi hadi nchi kuanzia miaka ya 1950 kwa Afrika kusini na Congo, miaka ya 1960 Zambia na Zimbabwe, miaka ya 1975 Afrika Kusini na Msumbiji na 1995 Afrika Kusini na Zimbabwe.

Nchi wanachama wa Sub Sahara Afrika Power Pools (SAPP) kumi na mbili kama zifuatazo;
Botswana Power Corporation (BPC).
Electricidade de Mocambique (EDM)
Empresa Nacional de Electricidale (ENE) OF Angola
Electricity Supply of Commission (MESC) of Malawi
Eskom of the Republic of South Afrika
Lesotho Electricity Corporation (LEC)
Nam Power of Nambia
Societe Nationale d' Electricate (SNE) of the DRC
Swaziland Electricty Board (SEB)
Tanzania Electric Supply Company ltd (Tanesco)
Zambia Electricty Supply Corporation (ZESCO)
Zimbabwe Electricty Supply Authority (ZESA)

Mradi muhimu ya SAPP ni tatu
1-Kutengeneza umeme ulipo kupunguza na kusambaza umeme sehemu zingine kwa kuanzisha miradi ya muda mfupi ya umeme kanzia 2004-2006
2-Kuongeza mradi kwa madhumuni ya kuungunisha umeme kati ya wanachama Malawi-Msumbiji na Zambi –Tanzania
3-Mradi ya muda mrefu kati ya 'Western Corridor Project –DRC,Angola, Nambia,Botswana na Afrika Kusini, Eastern Cirridor ya Afrika Kusini Mozambique, Malawi, Tanzania, Kenya na Uganda

Mnamo Aprili EAC- Kenya, Uganda na Tanzania waliazimia kwamba mpaka mwaka 2011 watakuwa na umeme wa kuchngia ili kupunguza upungufu wa umeme uliopo katika nchi yenye umeme mwimgi kwaenda nchi yenye upungufu wa umeme kwa kutoa kipawa mbele kwa nchi za

- Kenya (Lessos)- Uganda (Jinja)
- Ethiopia – Kenya
- Ethiopia –Sadan –Egypt
- Zambia-Tanzania- Kenya
- Rwanda (Ruzizi) – DRC

Nchi za EAC mfano wa Kenya na Uganda wamekuwa wakichangia umeme kwa muda mrefu "bilatera agreement kuuza na DRC –Rwanda na Burudi 'bilatera agreement'.
Wafadhali wa miradi ya umeme kwa SSA ni USAID katika kusaidia kusambaza umeme nchi za SSA kuwa na umeme wa kutosha. USAID wamekuwa wakitoa msaada ya mradi ya umeme kuanzia mwaka 200-2005 na imekuwa na majadiliano na wataalamu katika umeme wa power pools na inasaidia fedha kwa ajili ya mikutano na masuala mengine yanayohusu umeme.

Mada ya namna ya kujenga Mfumo wa Elimu ambao utawaandaa Vijana wa nchi za Afrika kutumia elimu hiyo katika kukabiliana mabadiliko ya technolojia duniani uliongoza na waziri wa Elimu ya Juu Sanyansi

Changamoto katika Elimu:

Upungufu wa vifaa vya kufundishai

- Upungufu wa walimu na watalaamu wengine
- Ukosefu wa fedha kwa ajili ya kuendesha sekta ya Elimu
- Viongozi wa serikali kuwa na urasimu
- Upungufu wa Vyuo mbalimbali na Vyuo vikuu
-

Mikakati ya Serikali:

Kuongeza vyuo vikuu, vyuo vya ufundi, vyuo vya elimu ya Jamii

- Kuboresha huduma zinazotolewa na sekta ya Elimu
- Uwezekano wa katika masomo ya Sayansi na Teknologia kukithi mahitaji kufuatana na utandawazi
- Kuwekeza katika sayansi na teknolegia na nchi nyingine – Amerika.

Mada ya Waafrika wanaoishi nje ya Afrika (Diaspora) katika uwekezaji, uraia na uhusiano wa kindugu:

Mch. Jessy aliongoza majadiliano ya mada hiyo kwa kusema kwamba ili tuweze kuamuniana katika kufanya biashara pamoja, kuwekeza katika Makampuni kwa pamoja ni budi tuweze kutambuana kiundugu kwa sababu sisi tulitoka Afrka kwa njia ya utumwa na kwa sababu hiyo Afrika ndiyo nyumbani kwetu, waliomba kuwa na uraia wa nchi mbili, ili kuweza kushirikiana katika kuijenga na kuja Afrika bila masharti kwa kutambua kuwa sisi sote ni ndugu wa damu, wajumbe kutoka Afrika walisema wanatambua uhusiano huo lakini sheria zinampaka yake katika saula la uraia wa nchi mbili.

Katika majadiliano hayo wajumbe kutoka nchi za Afrika waliomba Diaspora pamoja na marafiki wengine wa Afrika kuendeleza Afrika kwa kutumia taaluma zao kama za sayansi, walimu, uhandisi na n.k. Kujitolea katika familia au kiukoo katika kuendeleza maendeleo ya Afrika kama ndugu moja.

Aidha Waliomba umoja wa Afrika kuanzisha mkoa mwingine nje kwa ajili ya wamerikani weusi Ili kuweza kujenga mahusiano ya karibu, kurudiana tena kama ndugu moja katika ujenzi wa Afrika. Kuwepo urafiki kijiji kwa kijiji, taasisi na taasisi na shule na shule na Afrika Diaspora, Kuwa na matandao wa kutuunganisha waafrika wote duniani.

04-6-2008

Mada - kutangaza Utalii katika Afrika iliongozwa na Waziri wa Utalii Mhe. Shamsa Mwangunga, kuhusu jinsi nchi za Afrika zinavyoweza kukuza Utalii.

Alianza kwa kuwambia wajumbe ya kwamba katika mwaka 2007, utalii ilikuwa kwa kiasi cha 8.1% katika dunia. Utalii katika Afrika ni sekta ya pili kama chanzo cha mapato. Pamoja na vivutio vikubwa vilivyopo vinavyovutia utalii kama hali ya hewa, mazingira ya aina mbalimbali, miti na wanyama, historia, utamaduni fursa za biashara, makabila na tamaduni aina mbalimbali, miuundo ya majengo kama Pyramidi n.k. Kadhalika kikuu zipo changamoto mbalimbali zinazokabili sekta ya utalii,ni pamoja na umbali, ukosefu wa usafiri, ukosefu wa hoteli nzuri, gharama za usafiri hoteli na 'lodging'.

Afrika ni nchi inayofikiriwa na watalii kutoka nchi mbalimbali ni mbali sana, hakuna usafiri wa ndege, kuwa safari ni ndefu sana, na bei ya tiketi ni kubwa sana inafanya wengi kushindwa kufanya utalii Afrika. Mwaka 2007 utalii Afrika ulikuwa kwa 10% kwa wastani wa watalii 44m kutoka nchi mbalimbali duniani. Vivutio vya watalii ni kama mbuga za wanyama na 'eco-toursm', utamaduni na 'hertage toursm', maajabu, michezo, "recreational toursm", mikutano, Utalii.

Sera za kutangaza Utalii Afrika ni kama ifuatavyo:

- Kutangaza utalii kwa nguzu zote
- Kuboresha mazingira ya Utalii
- Kutunza na kuweka na kuifadhi utamaduni na sehemu za historia.
- Kuwekeza katika muundo mbinu
- Kufanya mipango kampeni za Utalii
- Kuhakikisha usalama na ulinzi Protocal kwa watalii
- Utali kuunganisha huduma za utalii katika nchi za Afrika

Changamoto katika sekta ya utalii Tanzania:

- Kutokujulikana kwa fursa ya masoko ya utalii nchi za nje
- Kutokuwa na ubora kwa huduma na kuongezeka kwa dhamani ya fedha
- Ushindani wa utalii Tanzania kulinganisha nchi za Afrika na duniani.
- Mgawanyo wa mapato ya fedha yanatokana na Utalii kwa jamii.
- Usafiri wa barabara na ndege kwa watalii
- Hali ngumu ya mazingira ya Tanzania

Fursa katika sekta ya Utalii Tanzania:

- Kuwekeza katika huduma za mahoteli yaliyopo na mapya.
- Kutekeleza sera za serikali kwa kutanganza na kuboresha utalii. Kuvutia utalii nchi na nchi kufuatana na mwingiliano kwa faida ya ubia.
- Kuweka nguvu kwa kuhusisha wizara ya mazingira Bodi ya Utalii, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko,Wizara ya Fedha, Wizara ya Miundo mbinu katika kutanganza na kuboresha mazingira ya utalii na kuandaa master plan katika utalii.
-
- Katika kujadili mada hiyo wajumbe kwa ujumla walisema kwa kuwa Tanzania ni nchi yenye ya nchi mbayo haina migogoro na vita vya kikabila, yenye msingi imara ya demokrasi katika kutoa kipawa mbele katika vivutio vya uwekezaji, biashara katika utalii na usafiri.
- Maeneo ambayo yanatiliwa mkazo ni pamoja na kuongeza uwekezaji katika utalii na kujitahidi kuboresha huduma bora katika miundo mbinu usafiri wa njia ya ndege na barabara, hoteli na sehemu za malazi.
- kufanya bidii katika kampeni za kutangaza masoko ya utalii kwa ajili vivutio katika kuwekeza katika utali.i
- Kutafuta uvumbuzi wa changamoto na fursa ili kuleta mafanikio makubwa yanapatikana katika kukuza uchumi kutokana na sekta ya utalii.

Mada ya mipango iliyofanya Utalii kuwa na mafanikio katika nchi ya Jamaica

Mada hii iliongozwa na H.E. P.J. Petterson aliyekuwa Mkuu wa Jamaica, katika majadiliano hayo taarifa ilitolewa jinsi Jamaica ilivyofanikiwa katika sekta ya utalii kwa kutumia fursa zizokuwepo. Utalii katika uchumi wa Jamaica una fursa kubwa katika ushindani wa biashara soko la nje, utalii unatoa fursa za kiuchumi kwa maisha ya watu wa kawaida. Ni sekta yenye kuwa na nguvu katika maisha ya maendeleo ya uchumi wa Jamaica.
Aliwaeleza wajumbe kwamba Jamaica imebarikiwa kuwa na mazingira mazuri ya maeneo ya utalii sehemu za heritage, entertaiment sports na traditional area ,sun na sand. Bodi ya utalii ilitangaza maeneo yake ya utalii kwa kutumia misamiati ya maneno ya biashara kwa kusema kwamba "**ONCE YOU GO YOU KNOW".**

Jinsi mandeleo ya Utalii yalivyoanza Jamaica; walianza kwa kutengeneza sehemu zenye kuvutia kwa ajili ya mapumziko kwa watu maarufu na matajiri kutoka nchi za ulaya na Amerika.

Kutangaza fursa za mazingira ya milima mizuri ilizunguka Jamaica, majengo makubwa nje ya mji kwa mapumziko binafsi, wageni wa coca cola na wengine hotel ndogo zenye masoko ya kuvutia.
Njia zilizotumika katika kuleta mafanikio ya utalii Jamaica
Mikutano ya wadau katika kutengeneza matangazo wenye ujumbe wa kuvutia watalii
Kutangaza utalii kwa kupeleka ujumbe wenye kusema sifa za ukweli na uwazi wa kuhusu bidhaa ya utalii Jamaica
Kufanya mawasiliano kuhusu utalii ambayo yataleta matokeo mazuri
Kutoa taarifa sahihi zenye kuonyesha maelezo yenye kukubalika na kuheshimika
Kutoa motisha kwa watembeza wageni
Kuwekea watalii huduma nzuri zenye kuvutia na uaminifu ili kuvutia watalii wapya

Mikakati muhumu iliyofanikisha maendeleo ya Utalii Jamaica
Kuwekeza kwa hali ya juu katika rasilimali watu
Kuwa na miundo mbinu mizuri, daraja la kwanza, baraba, viwanja vya ndege, bandari miundo ya mawasiliano na taarifa , nishati, maji na mifumo mizuri ya maji taka
Kuwa na uwazi katika uchumi wa nchi katika kuwanufaisha watu wote
Ubora wa utendaji kazi katika sekta binafsi na umma inayolenga katka ubunifu na utamaduni
Kuweka uwazi kazi za sekta ya umma na katika uchumi wa nchi
Kuwa na sheria zenye kulinda na kutetea mali, haki za binadamu na mahusiano ya jamii kuwa imara
Kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na kwa watalii

“Presidential Plenary”

Majadiliano aliongozwa na mwenyeji wa mkutano Rais J. M. Kikwete kwa kuelezea sekta zinazohitaji wawekezaji kutoka nje kuwekeza katika Utalii kama nguzo kuu ya uchumi ya mapato ya afrika na afrika ikiwa ya kwanza kupokea Watalii duniani , Sekta hiyo imekuwa ikikabiliwa na miundo mbinu hafifu kama barabara, bandari na ndege kwa ajili ya Utalii. Ili kuboresha miundo mbinu hiyo tunahitaji uwekezaji mkubwa. Kutokana na idadi kubwa ya watalii wanaokuja Afrika kuona vivutio vya Utalii vilivyopo na ambayo havipo katika mabara mengine duniani.

Naye Rais Paul Kagame wa Ruwanda katika aliwaambia wajumbe kwamba Bara la Afrika linashindwa kukua kiuchumi kwa kukwamishwa kutoka na vikwazo mbalimbli vya rushwa, urasimu vita na utaratibu za mingiliano katika nchi na

nchi za bandari ambayo huongeza gharama za uzalishaji na kuongeza umaskini barani Afrika .

Rais wa Msumbuji Amando Gweyebuza aliwambia wajumbe kwamba matatizo kubwa linalokabili Afrika ni umaskini uliosababishwa na ukoloni na unyonyaji kwa bara hili, limeendelea kuwa maskini hata baada ya kupata Uhuru miaka kadha sasa, Serikali za Afrika zinapaswa kukaa na wananchi waliopo Vijiji na kujadiliana kwa pamoja namna ya kuwakomboa/kushughulikia umaskini kwani wao ndiyo waathirika wakubwa katika uchumu.

Aidha Afrika ibadili mtazamo au mbinu za kushughuliki matatizo kulingana na mazingira yaliyopo kwa kushirikisha wananchi wa vijiji kufanya hivyo kutabadilisha Afrika katika maendeleo yake.

Rais wa Kenya Mwaki Kibaki alitoa fursa nyingi za kuwekeza katika nchi ya Kenya na Afrika kwa ujumla katika utalii, Miundo Mbinu, ujenzi wa mahoteli makubwa, mawasiliano, nishati ya umeme na jua, huduma za jamii na sekta ya kilimo n.k.

Rais Abdelezizi Boutethka wa Algeria alisema yafuatayo mkutano huu wa sullivan uwe ni changamoto katika “identifying and explorting trade” na fursa za uwekezaji kati ya bara la afrika na bara mengine na hasa Waafrika Diaspera wa Merikani, ni vizuri bara la Afrika waomba Diaspora kusaidia bara hili kutokana na changamoto za Maendeleoo kutokana na “theme” ya mkutano huu ya utalii na maendeleo ya Miundo mbinu kama misingi madhubuti wa kutatua changamoto hizo na mkutano huu imekuja wakati Afrika inajipanga kutumia rasilimali muhimu katika maendeleo yake na kuhakikisha imetumia malengo yake na mabara mengine.

Maraisi wenigine walizumzia jinsi Afrika inapaswa kujipanga kwa kutumia umoja wao na pia kwa kuwaomba Afrika Diaspora na marafiki wengine wanaoipenda Afrika kuwekekeza katika fursa mbalimbali za uchumi. Aidha Mkutano wa Leon sullivan utasaidia katika kuwezesha Afrika kuwa na nguvu moja katika kuwawezesha kimaendeleo.

Afrika inahitaji wawekezaji katika sekta ya Viwanda, kilimo na utalii ambapo maendeleo yetu yanategemea sana, sera nzuri tayari zinaandaliwa ili kuwavutia wawekezaji, zipo fursa za ardhi, kufanya bara la Afrika kuwa na ushindani kiuchumi, vile vile vipo vivutio vya kitalii vinayohitaji kuendeleza kwa ajili ya kupata utajiri na kazi na mfano wa utalii uliopo Afrika ni mwenyeji wa Mkutano huu ambao umejionea wenyewe katika sehumu mbalimbali za utalii Tanzania.

Marais wote sifa waliwaalika wamerikani Diaspora kuja kuwekeza Afrika katika sekta mbalimbali za kiuchumi kwa kuzingatia wao wamepiga hatua kiuchumi na ni ndugu wa Afrika na wana uchungu na hali ya umaskini uliopo Afrika.